# MWONGODHO WA MWALIMU
# GIREDI 3

Yumna Hamid Titi
Fuad Aroi
Yumbe Athman

TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road, Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-21-8**

Kitabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

In partnership with

BRITISH COUNCIL

Department for Culture, Media & Sport

# Yaliyomo

1. Vanyama Va Mwichuni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2. Usalama Barabarani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

3. Kadhi Mbalimbali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 12

4. Machumidhi A Mayi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17

5. Misimu Mbalimbali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwatoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia twavashukuru vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Novemba, 2023

# 1 VANYAMA VA MWICHUNI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: DHILIO DHA VANYAMA VA MWICHUNI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuchaya mayina a vanyama va mwichuni.
- Awedhe kudhichambua sauṯi dha vanyama mbalimbali va mwichuni.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi 3 ukurasa wa 1

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha dha vanyama, kifaa cha kidijitali.

**Swali ḏaḏisi:** Vanyama va mwichuni huchusaidia nini?

**Uṯaraṯibu wa Kufundrisha**

- Mwalimu avavulidhe maswali vanafunḏi kuhusu vanyama va mwichuni k.m: nnyama haṯari mwichuni ni upi?
- Vanafunḏi vadhungumudhe kuhusu vanyama.
- Mwalimu avasikidhishe sauṯi mbalimbali dha vanyama akichumia kifaa cha kidijitali, vanafunḏi vadhichambue sauti hidho.
- Vaongodhe kuangalia picha ukurasa wa 1 vachaye mayina a vanyama.
- Vashirikishe vanafunḏi kuṯaba sauṯi dha vanyama na vangine vadhichambue.
- Vanafunḏi vachore nnyama wa mwichuni vampenḏae.

## ISOMO LA PILI

**MAḏA KURU: KUDHUNGUMUDHA**

**MAḏA NDRODI: UMUHIMU WA VANYAMA VA MWICHUNI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kutoa ujumbe kwa kuchumia picha dhilidhoko kiṯabuni.
- Kuchaya mayina a vanyama na umuhimu wavo.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha vanafunḏi uk. 2

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kaḏi-maneno, kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Vanyama va mwichuni vana umuhimu gani kwechu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vakumbuse vanafunḏi kuhusu vanyama va mwichuni valivosoma kachika isomo lililopicha.
- Vaongodhe vanafunḏi kuangalia picha dhiṯabuni kueledhea vakivonacho.
- Vape nafasi vanafunḏi vajalidiliane kuhusu umuhimu wa vanyama va mwichuni kachika dhikundri.
- Orodhesha umuhimu wa vanyama va mwichuni ubavoni vanafunḏi vasome kwa sauṯi.

## ISOMO LA CHACHU

**MAḏA KURU: KUDHUNGUMUDHA**

**MAḏA NDRODI: KULINDRA VANYAMA VA MWICHUNI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchaya sampuli mbalimbali dha kuvalindra vanyama va mwichuni.
- Kueledha umuhimu wa vanyama va mwichuni

- Kufurahia vanyama va mwichuni.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha vanafunḏi uk. 2

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati, kifaa cha kidijitali

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vashirikishe vanafunḏi kukumbuka umuhimu wa vanyama va mwichuni.
- Vaveke vanafunḏi kachika dhikundri vachaye namuna a kuvahifadhi vanyama va mwichuni.
- Vanafunḏi vasome maeledho kachika chati.
- Vanafunḏi vakaṯafudhe ndia dhaiḏi dha kuvalindra vanyama va mwichuni.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: HIFADHI DHA VANYAMA VA MWICHUNI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchaya naamuna mbalimbali dha kuhifadhi vanyama va mwichuni
- Kusoma madhungumudho na kujibu maswali
- Kufurahia kusoma madhungumudho

**Marejeleo:**Kiṯabu cha vanafunḏi uk. 3 na 4

**Dhifaa dha kufundrishia:** Picha dha vavindaji na vanyama, kifaa cha kidijitali.

**Swali ḏaḏisi:** Kwa nini vanafunḏi hupekwa matembedhi kwene hifadhi a vanyama va mwichuni?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kueledhea kuhusu picha.

- Vanafunḏi vachaye vanyama vavindhwavo.
- Vanafunḏi vasome madhungumudho kiṯabuni.
- Vanafunḏi vaeledheane kuhusu madhungumudho.
- Vanafunḏi vajibu maswali.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUUNDRA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kupanga maneno kuundra senchensi sawa
- Kusoma senchensi kwa udhuri
- Kufurahia kuundra na kusoma senchensi

**Marejeleo:**Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 5

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kaḏi-maneno, chati

**Swali ḏaḏisi:** Senchensi huundrwaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaongodhe vanafunḏi kusoma maneno kwa usawa.
- Vanafunḏi vasome maneno kachika kaḏi dha maneno.
- Vaongodhe kuchumia kaḏi maneno kupanga senchensi.
- Vaongodhe kusoma senchensi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vaundre senchensi zaiḏi dhiṯabuni.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Makadhi a vanyama
2. simba, nachi, tuvi, pisi
3. simba

4. Vasivuwawe, huecha senti dha kigeni
5. majangili

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUCHUNGA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchunga senchensi kuhusu ulindraji wa vanyama pori.
- Kusoma senchensi kwa udhuri
- Kufurahia kuchunga na kusoma senchensi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 5.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Mfalume wa vanyama va mwichuni ni nyanyi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaongodhe vanafunḏi kusoma maneno kweṉe kaḏi.
- Vaongodhe vanafunḏi vapange maneno kuchengedha senchensi.
- Mwalimu avasaiḏie vanafunḏi kuundra senchensi.
- Vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vaanḏike senchensi dhiṯabuni.

# 2 USALAMA BARABARANI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: HAḎISI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusimulia haḏisi
- Kusikidha haḏisi
- Kufurahia kusimulia na kusikidha haḏisi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.7

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhiṯabu dha haḏisi, Kifaa cha kidijitali.

**Swali ḏaḏisi:** Kwa nini chwaṯakiwa chuve vaangalifu barabarani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha umuhimu wa kuva makini barabarani.
- Vanafunḏi vajaḏili nchoro ulioko kiṯabuni uk.7.
- Mwalimu asimulie hadisi fupi kuhusu usalama wa barabarani.
- Aagidhe vanafunḏi vasimuliane hadisi fupifupi kachika makundri.
- Mwalimu avase kifaa cha kidijitali na avaagidhe vanafunḏi vanyamae ili vasikidhe hadisi kwa uchulivu.
- Mwalimu avavudhe maswali kuṯokana na hadisi valosikidha.

## ISOMO LA PILI

### MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

**MAḎA NDRODI: USHAIRI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kufikia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma shairi
- Kukariri shairi kwa mahadhi
- Kufurahia kusoma na kukariri shairi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 8

**Dhifaa dha Kufundrishia:** Chati, Kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Ni alama gani vachu hufaa kuvuka kachika barabara?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu barabara.
- Mwalimu asome shairi na alikariri kwa mahadhi
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue uk. 8 ili vasome shairi kwa sauṯi.
- Vanafunḏi vanṯabe mwalimu akikariri shairi.
- Angika chati ubavoni, vanafunḏi vachambue alama a pundra milia.
- Vaeledhe umuhimu wa alama hiyo.
- Hitimisha isomo kwa kueledhea ujumbe umuhimu kweṉe shairi hilo.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA KURU: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: UFAHAMU (SHARIA DHA BARABARANI)**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:-

- Kusoma ufahamu kwa udhuri
- Kujibu maswali a ufahamu
- Kufurahia kusoma ufahamu

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.9

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali, chati

**Swali ḏaḏisi:** Ni sharia gani dha barabarani udhiyivadho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kurejelea isomo lililopicha kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu usalama barabarani.
- Vaagidhe vanafunḏi vafungue dhiṯabu uk.9 ili vajaḏili picha.
- Mwalimu asome kifungu cha kwanḏa kwa sauṯi.
- Vaagidhe vanafunḏi vasome ufahamu kwa sauṯi.
- Angika chaṯi ubavoni na aeledhe umuhimu wa ṯaa dha barabara.
- Ahiṯimishe isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu maswali.

## Majibu alopenḏekedhwa:

1. Makini, tahadhari, mwangalifu
2. Kulia na kusoṯo
3. Daraja la kuvukia, kuvuka kweṉe alama dha pundra milia, kuangalia michoro a tahadhari.
4. Leseni
5. Maovu

## ISOMO LA IṈE

**MAḎA KURU: KUSOMA**

### MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma senchensi kwa udhuri
- Kufurahia kusoma senchensi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 11.

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chaṯi

**Swali ḏaḏisi:** Ni sehemu gani salama dha kuvuka barabara?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu barabara.
- Mwalimu aagidhe vanafundi vafungue uk wa 11
- Mwalimu asome senchensi kwa sauṯi na vanafunḏi vamuanḏame akisoma.
- Kachika makundri, vanafunḏi vasome senchensi hidho kwa sauṯi.
- Hiṯimisha isomo kwa kuangika chaṯi ubavoni ili vanafunḏi vasome.

## ISOMO LA ṮANU

**MAḎA KURU: KUANḎIKA**

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika senchensi kwa udhuri
- Kufurahia kuanḏika senchensi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.11

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kadi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Ni alama dhipi dha barabarani udhiyivadho?

**Uṯaraṯibu wa Kufundrisha**

- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi vasome maneno kweṉe kadi.
- Mwalimu aundre senchensi kuchumia ineno imoya kweṉe kadi na alianḏike ubavoni.
- Avaagidhe vanafunḏi vafungue dhiṯabu uk.11 vasome hao maneno.
- Vanafunḏi vachunge senchensi vakichumia maneno hao.
- Hiṯimisha isomo kwa kurekebisha senchensi hidho pamoya na vanafunḏi.

## ISOMO LA SIṮA

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUANḎIKA NCHUNGO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika nchungo ndhuri.
- Kufurahia kuanḏika nchungo.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.11

**Dhifaa dha Kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Nchungo ni nini?

**Uṯaraṯibu wa Kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha maana a nchungo.
- Mwalimu avaeledhe namuna a kuanḏika nchungo weṉe nṯiririko ndhuri na wa kueleweka.

- Avase kifaa cha kidijitali avavoneshe vanafunḏi nfano wa nchungo ndhuri.
- Avaagidhe vaanḏike nchungo kuhusu usalama barabarani.
- Hiṯimisha isomo kwa kusisiṯidha vaanḏike misemo na mesali kweṉe nchungo.

# 3 KADHI MBALIMBALI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: KADHI MBALIMBALI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kuchaya kadhi mbalimbali
- Kuṯaba kadhi dha aina mbalimbali

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa 12

**Dhifaa dha kufundrishia:** Michoro, kaḏi-maneno, kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Je, kuna umuhimu wa vachu kufanya kadhi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vavulidhe vanafunḏi kadhi dha vadhadhi vavo.
- Vavulidhe vanafunḏi vangepenḏa kufanya kadhi gani vakiva vakuru.
- Vaongodhe kufungua kiṯabu ukurasa wa 12 ili kujaḏili michoro iliyoko kiṯabuni.
- Vaongodhe kuchaya kadhi mbalimbali dha kikwechu.
- Vaṯabe kadhi mbalimbali vakichumia picha kiṯabuni.

## ISOMO LA PILI

### MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KUṮABA KADHI MBALIMBALI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kuṯaba kadhi mbalimbali.
- Kufurahia umuhimu wa kufanya kadhi.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk- 13

**Dhifaa dha kufundrishia:**Kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Ni kadhi gani dhifanywadho kachika maeneo echu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaongodhe vanafunḏi kuchaya kadhi ambadho vadhipenḏadho.
- Vaavanye vanafunḏi kachika makundri mbalimbali.
- Liongodhe ikundri imoya imoya kuṯaba shuhuli dha kadhi hidho.
- Vapongedhe vanafunḏi kwa kushiriki kachika maigidho hao.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI:  USHAIRI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kusoma shairi kwa udhuri.
- Kukariri shairi kwa mahadhi madhuri.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk- 13

**Dhifaa dha kufundrishia:**Kifaa cha kidijitali, chati.

**Swali ḏaḏisi:** Mashairi huchusaidiaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi kukariri shairi lolote valiivalo.
- Soma shairi uk. 13 kwa sauṯi na mahadhi, vanafunḏi vasikidhe kwa makini.
- Vaongodhe vanafunḏi kulisoma na kulikariri shairi hilo.
- Vaavanye kimakundri na vakariri shairi hilo.
- Vaongodhe kuchaya kadhi dhilodhungumudhiwa kweṉe shairi.

## ISOMO LA INE

**MAḎA KURU: UFAHAMU**

**MAḎA NDRODI: UṮONYI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kusoma ufahamu kwa udhuri
- Kujibu maswali a ufahamu
- Kufurahia kusoma ufahamu

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk-14

**Dhifaa dha kufundrishia:** Michoro, kaḏi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Utonyi ni kadhi aina gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrishia**

- Vaongodhe kujadili nchoro ulioko kiṯabuni uk.14
- Soma kifungu cha kwanḏa kwa sauṯi.
- Ṯaua mwanafunḏi asome kifungu cha  pili na vangine vamalidhe.
- Vaeledhe maana a maneno magumu.
- Vaongodhe kujibu maswali alioko kiṯabuni.

**Majibu alopendekedhwa:**

1. Baharini, nchoni au idhivani.
2. Majarifa, nyavu, mayema, nshipi na juya.
3. Kichoveo, huecha senti dha kigeni
4. Kamba, mayongoo, kaa
5. majibu ṯafauṯi a vanafunḏi

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: IMLA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kusikidha kwa makini.
- Kuanḏika Imla bila makosa.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk-15

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Kusikidha kwa makini husaidia nini?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaṯayarishe vanafunḏi na dhifaa dha kuanḏikia.
- Vaeledhe vave vasikivu na vachulivu.
- Soma senchensi kwa umakinifu na kwa sauṯi.
- Rudia senchensi hidho mara a pili.
- Dhunguka na kuangalia kadhi dha vanafunḏi vakiandika haṯi nadhwifu.
- Vapongedhe valivoanḏika kwa udhuri.

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: NCHUNGO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kuanḏika nchungo kwa haṯi nadhwifu.
- Kufurahia kuanḏika nchungo.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk-15

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali, chati.

**Swali ḏaḏisi:** Ungalipenda kufanya kadhi gani ukiva nkuru?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaeledhe vanafunḏi kuhusu kadhi mbalimbali dhifanywadho sehemu dhechu
- Vasomee nfano wa nchungo ulioko kweṉe kifaa cha kidijitali kuhusu kadhi mbalimbali.
- Vaongodhe vanafunḏi kwa kuvaandikia dhipengee mbalimbali.
- Vaongodhe vanafunḏi kuanḏika nchungo wa kadhi aipenḏao.
- Soma nchungo wa vanafunḏi kadhaa ili kuwedha kurekebisha.

# 4 MACHUMIDHI A MAYI

## ISOMO LA KWANḏA

**MAḏA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḏA NDRODI: MACHUMIDHI A MAYI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe;

- Kuchaya machumidhi a mayi
- Asikidhe haḏisi kwa makini

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk-16

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kifaa cha kidijitali, Chaṯi.

**Swali ḏaḏisi:** Mayi huchumiwaye ṉumbani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu machumidhi a mayi
- Vanafunḏi vafungue kiṯabu uk.16 ili vajadili picha.
- Mwalimu aṯoe kifaa cha kidijitali na avavoneshe vanafunḏi picha na video dha machumidhi a mayi.
- Mwalimu asimulie haḏisi kuhusu machumidhi a mayi.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu hadisi valosikidha.

## ISOMO LA PILI

### MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: MADHUNGUMUDHO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusikidha madhungumudho kwa makini.
- Kuchaya machumidhi mbalimbali a mayi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk-17

**Dhifaa dha Kufundrishia:** Michoro

**Swali ḏaḏisi:** Mayi ana umuhimu gani kwa binadamu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha machumidhi mbalimbali a mayi.
- Avaagidhe vanafunḏi vafungue kitabu uk. 17 ili vajadili michoro.
- Vashirikishe vanafunḏi kweṉe madhungumudho.
- Vanafunḏi vasome madhungumudho kachika makundri.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: UFAHAMU (MAYI NI UHAI)

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma ufahamu kwa udhuri.
- Kujibu maswali.
- Kufurahia kusoma.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 18

**Dhifaa dha kufundrishia:** Kaḏi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Kwa nini mayi ni uhai?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha umuhimu wa mayi.
- Angika kaḏi-maneno vanafunḏi vasome.
- Mwalimu asome ufahamu kifungu cha kwanḏa kwa sauṯi uk.18.
- Kachika makundri, vaagidhe vanafunḏi vasome ufahamu kwa kupokedhanya.
- Hiṯimisha isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu maswali.

## Majibu alopendekedhwa

1. Uhai
2. Rabi, Mungu, Mola
3. Vua
4. Kukonga ruhu, kupikia, kusafisha nvili, kudhinya mocho, kusafirisha dhombo kama bochi, meli nk.
5. Isi, kamba, kasa, pomboo

## ISOMO LA INE

**MAḎA KURU: KUSOMA**

**MAḎA NDRODI : MESALI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma mesali kwa ufasaha
- Kuelewa maana dha mesali

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 19

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chaṯi

**Swali d̠ad̠isi:** Mesali ni nini?

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha maana a mesali.
- Mwalimu asome mesali kwa saut̠i uk.19
- Kachika makundri, vanafund̠i vasome mesali.
- Vanafund̠i vaeledheane maana dha mesali valosoma.
- Mwalimu ahit̠imishe isomo kwa kuand̠ika chati na vasome mesali kwa pamoya.

## ISOMO LA T̠ANU

## MAD̠A KURU: KUAND̠IKA

### MAD̠A NDRODI: UMOYA NA WINGI

**Mat̠okeo maalumu t̠arajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafund̠i awedhe:

- Kubadilisha senchensi kachika umoya na wingi.
- Kusoma senchensi kwa umoya na wingi
- Kufurahia kusoma na kuand̠ika senchensi

**Marejeleo:** Kit̠abu cha mwanafund̠i uk.19

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati

**Swali d̠ad̠isi:** Mayi huchimiwaye hondreni?

**Ut̠arat̠ibu wa Kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafund̠i maswali mbalimbali kuhusu mayi.
- Mwalimu avaeledhe vanafund̠i namuna a kubadilisha senchensi kut̠oka umoya kwa wingi na wingi kwa umoya.
- Mwalimu aangike chati ubavoni en̠e mifano a senchensi a umoya na wingi.

- Avashirikishe vanafunḏi vafungue kiṯabu uk. 20 ili vaanḏike senchensi kwa umoya na wingi kweṉe dhiṯabu dhavo.

**Majibu alopendekedhwa**

1. Mafunḏi huundra majahadhi.
2. Vakulima valinosea mimea.
3. Madau alidhama
4. Nguvo dhindofuliwa.
5. Dhombo dhilioswa kwa udhuri.
6. Dhisima dhifukudhiwa.
7. Madovo akachisie kamba.

## ISOMO LA SIṮA

### MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: NCHUNGO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika nchungo ndhuri
- Kufurahia kuanḏika nchungo

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.20

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati

**Swali ḏaḏisi:** Nchungo ndhuri huanḏikwae?

**Uṯaraṯibu wa Kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kueledha maana a kiṯwa cha nchungo.
- Mwalimu aeledhe dhipengee muhimu dha kuanḏika nchungo.
- Angika chaṯi ubavoni na avashirikishe vanafunḏi vasome mesali na semi ili vadhichumie kuanḏikia nchungo.

- Vaagidhe vanafunḏi vaanḏike nchungo kuhusu machumidhi a mayi.
- Vahimidhe vanafunḏi vaanḏike kwa haṯi nḏuri.
- Mwalimu avasomee vanafundi nchungo ndhuri.
- Vahamidhe kupenḏa kuanḏika nchungo ndhuri.

# 5 MISIMU MBALIMBALI

## ISOMO LA KWAN<u>D</u>A

**MA<u>D</u>A KURU: KUSIKIDHA**

**MA<u>D</u>A NDRODI: MISIMU MBALIMBALI**

**Ma<u>t</u>okeo maalumu <u>t</u>arajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafun<u>d</u>i awedhe:

- Kuchambua misimu mbalimbali kachika mwaka.
- Kuchaya shuhuli dhifanywadho kachika misimu mbalimbali.

**Marejeleo:** Ki<u>t</u>abu cha mwanafun<u>d</u>i ukurasa wa 21

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati, kifaa cha kidijitali, kadi-maneno

**Swali <u>d</u>a<u>d</u>isi**: Misimu ni nini? Utachambuaye misimu mbalimbali a mwaka?

**U<u>t</u>ara<u>t</u>ibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaavanye vanafun<u>d</u>i kwa dhikundri.
- Vaongodhe vanafun<u>d</u>i kudhungumudha kuhusu picha dhi<u>t</u>abuni ukurasa 21.
- Vanafun<u>d</u>i vaeledhane alioko kwe<u>n</u>e picha.
- Mwalimu avachayie misimu mbalimbali akichumia kadi-maneno.
- Vanafun<u>d</u>i vachambue misimu mbalimbali na shughuli dhifanyikadho kachika kila nsimu.
- Vanafun<u>d</u>i vaimbe nyimbo ichayadho misimu.

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: NJAḎALA

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kuchaya faida dha nsimu wa vua na yuva
- Kushiriki kachika njaḏala
- Kufurahia kushindrana kachika njaḏala

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 22

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi**: Njaḏala ni nini? Njaḏala hufanywaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avavulidhe vanafunḏi kueledha maana a njaḏala. Vanafunḏi vaeledheane.
- Mwalimu afafanue dhaidi maana a njaḏala.
- Avasikidhishe njaḏala kachika kifaa cha kidijitali.
- Vaavanye vanafunḏi kachika makundri mavili vajadili njaḏala ‘nsimu wa vua ni bora kuliko wa yuva’.
- Vanafunḏi vajadiliane na kushindrana vakifuacha masharuti a njaḏala.
- Mwalimu avasifu vanafunḏi valivoshiriki na avahimidhe vangine vashiriki kachika njaḏala.
- Mwalimu adhisome hoja dha vanafunḏi. Vanafunḏi vadhisome kwa sauti.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: UFAHAMU

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma kwa sauṯi
- Kujibu maswali a ufahamu
- Kusoma kwa udhuri na kufurahia

**Swali ḏaḏisi**: Ni shuhuli gani hufanywa kwen̠e misimu mbalimbali?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 22

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi dha misimu, chati, kadi-maneno

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha isomo kwa kuvakumbusa vanafunḏi kuchaya misimu mbalimbali.
- Mwalimu avaeledha vanafunḏi namuna a kuva nsomi ndhuri.
- Vaeledhe uṯaraṯibu wa kusoma kwa udhuri.
- Vaagidhe vanafunḏi kufungua ukurasa wa 22-23, Vape muda vadhungumudhe kuhusu picha.
- Vaongodhe kusoma kwa udhuri kimwakimwa. Kisha vasome kwa sauṯi vakipokedhanya.
- Vasaidie vanafunḏi kuchambua maneno mapiya, vaeledhe maana ake. Chumia kadi-maneno kuvavonesha vanafunḏi maneno mapiya.
- Vasifu vanafunḏi na uvahimidhe kupenḏa kusoma.

**Majibu alopendekedhwa**

1. Ni kipindri kachika mwaka ambapo hali maalumu a hewa hupachikana.
2. Nsimu wa kiangadhi/yuva, kusi/vua, dhoruba/upepo, vua rasharasha.
3. Nsimu wa dhoruba/upepo
4. Kusi/vua
5. Baridi kali

## ISOMO LA IṈE

### MAḎA KURU: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: KUSOMA SENCHENSI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kusoma senchensi kwa udhuri
- Kuchaya misimu mbalimbali

**Swali ḏaḏisi**: Ni shuhuli gani hufanyika nsimu wa vua?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 23

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi dha senchensi

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kwa kuvaelekedha vanafunḏi mambo a kudhingatia wakaṯi wa kusoma.
- Vashirikishe vanafunḏi kachika kusoma senchensi.
- Kachika dhikundri vanafunḏi vasome senchensi kuchumia kadi-maneno.
- Vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi dhiṯabuni uk.23.
- Vahimidhe Vanafunḏi kupenḏa kusoma mara kwa mara.

# ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: NRABA

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

- Kukamilisha nraba
- Afurahie kuyadha nraba

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 24

**Dhifaa dha kufundrishia**: Nraba, kadi dha misimu

**Swali ḏaḏisi:** Ni nsimu gani upendwao na vakulima?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vashirikishe vanafunḏi kuchaya misimu valosoma kipindri cha ṉima.
- Vavoneshe vanafunḏi kadi dhenye misimu mbalimbali.
- Vaongodhe vanafunḏi kuangalia nraba ukurasa wa 24. Vape maagidho a namuna a kuchambua maneno a misimu.
- Vanafunḏi vaṯafudhe maina a misimu kachika nraba.
- Vapongedhe vanafunḏi valivowedha kupacha maina ote mara moya.
- Rudia misimu ote pamoya na vanafunḏi kweṉe nraba.

**Majibu Alopenḏekedhwa:**

1. Kusi 2. Kiangadhi

3. Chaka 4. Dhoruba

5. Matlai

## ISOMO LA SIṮA

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: NCHUNGO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

- Kuanḏika nchungo ndhuri
- Kufurahia kuanḏika nchungo

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk.24

**Dhifaa dha kufundrishia:** Chati, mifano a michungo

**Swali ḏaḏisi:** Ni nsimu gani vanyama hudhoofika nno?

**Uṯaraṯibu wa Kufundrisha**

- Vaeledhe shuhuli dha misimu mbalimbali.
- Vasomee mifano a michungo mbalimbali.
- Vaandikie dhipengee mbalimbali kuhusu misimu.
- Kachika makundri vajadiliane dhipengee na vaandike nchungo kwa kusaidiana.
- Vape muda vanafunḏi vasome michungo avo mbee a darasa
- Rekebisha makosa a vanafunḏi.